USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

**Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI**

TOLEO NA. 6 AGOSTI-OKTOBA 2018




## Kuwezesha Mifumo Kuwasiliana katika Mikoa, Halmashauri na Vituo vya Kutolea Huduma

*Picha ya Mbele: Baadhi ya wataalam wa programu ya "Muungano Gateway" wakiwa katika kazi ya kuunda mifumo. Kutoka kushoto ni Bunto Mbozi, Nseya Kipilyango, Frank Kachinga na Chrispinus Melkiory (Picha:Maktaba)*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Angela Msimbira – TAMISEMI*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Angela Msimbira – TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Jacqueline Sombe – PS3*

## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri…………………………………………………………………………..uk 6**

**Muungano Gateway; Chanzo cha Maamuzi ya Kiutendaji Serikalini ……...uk 7**

**Muungano wa Mifumo Suluhu ya Ufanisi katika Vituo ...………..……...…..uk 8**

**Muungano Gateway Msingi wa Taratibu na Kanuni za Mifumo………...….uk 10**

**Matumizi ya Mifumo Yaokoa Zaidi ya Milioni 15 Kongwa………………….uk 11**

**Mifumo Thabiti Mhimili wa Huduma Bora kwa Wananchi………..……..……...uk 12**

**Tathmini na Ufuatiliaji Yarahisishiwa Upatikanaji Taarifa……………..….uk 13**

**Uwiano Sahihi wa Taarifa za Fedha Waimarishwa…………….....…………..uk 16**

## *TAHARIRI:*

# Mifumo Inayowasiliana ni Kiini cha Taarifa Sahihi

Mara kwa mara kumekuwa na ugumu katika upatikanaji wa taarifa zinazowiana kupitia mifumo ya utendaji ya TEHAMA iliyopo katika Halmashauri.

Mifumo inayotumika katika Halmashauri inategemeana kwa kiasi kikubwa, lakini kwa kipindi kirefu imekuwa ikifanya kazi kwa kujitegemea bila mawasiliano. Hii ililazimu zoezi la upatikanaji wa taarifa zinazotegemeana kuchukua muda mrefu kutokana na ukusanyaji wa taarifa hizo kuwa changamoto kubwa.

Kwa kutambua changamoto hizi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), imeamua kutengeneza mfumo unaounganisha mifumo yote unaojulikana kama *Muungano Gateway*, ambao ni mfumo wa Serikali unaowezesha mifumo mingine kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kurahisisha makutano ya mawasiliano baina ya mifumo ya ndani ya OR-TAMISEMI, Wizara za Kisekta na wadau wanaohitaji taarifa na takwimu mbalimbali.

Mifumo ambayo kwa sasa tayari imeunganishwa kutokana na taarifa zake kutegemeana kwa kiasi kikubwa, ni mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS), mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha kwa vituo vya kutolea huduma (FFARS), mfumo wa matumizi ya fedha za Serikali katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Toleo 10.2 (Epicor10.2), na mfumo wa mipango na bajeti (PlanRep).

*Muungano Gateway* ni njia ya msingi ya mifumo hii kuwasiliana na hivyo kuwezesha taarifa zinazotegemeana kupandishwa moja kwa moja '*automatically*' kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine. Hii inasaidia kuwa na taarifa zinazowiana na kuepusha makosa ambayo yangesababisha utofauti wa taarifa.

Mfumo huu utatoa nafasi kwa mifumo yote ya msingi iliyoko katika Halmashauri mpaka kufika kwenye ile iliyopo katika vituo vya kutolea huduma kupeana taarifa. Ni matarajio yetu kuwa watumiaji wa mifumo hii watakuwa wamerahisishiwa utendaji kazi katika kutafuta taarifa zinazotokana na mifumo mingine.

Jarida hili linatoa nafasi ya kufahamu namna gani mfumo wa *Muungano Gateway* unakwenda kutatua changamoto zilizokuwepo mwanzo kabla ya kuwepo kwa mfumo huu. Huduma zilizokuwa zinakwama na kuahirishwa kutokana na changamoto za kutokuwa na taarifa sahihi na muda mwingi kutumika katika kuzikusanya sasa zitasahaulika na wananchi wanaenda kufurahia huduma zilizoboreshwa.

Nawatakia usomaji mwema wa jarida hili na kwa pamoja tuendeleze gurudumu la maendeleo. Katika uboreshaji wa mifumo.

**Eng. Mussa Iyombe**

**Katibu Mkuu, OR -TAMISEMI**

# *Muungano Gateway:* Chanzo cha Maamuzi ya Kiutendaji Serikalini

Muungano wa mifumo (Interoperability) itasaidia mifumo ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kuwasiliana na kuwasaidia watoa maamuzi kutoa maamuzi kwa usahihi kulingana na uhitaji.

Inaelezwa kuwa upo umuhimu wa kufuata miongozo ya uwekaji mifumo nchini, miongozo ambayo itasaidia uwepo wa mifumo michache iliyounganika ambayo itajitosheleza katika utoaji wa huduma mbalimbali katika jamii.


Kuwepo kwa mifumo inafanya kazi pasipo kufanya kazi kila mmoja peke yake inasababishia Serikali gharama na uhitaji wa wataalam wengi, vifaa na fedha na usahihi wa taarifa.

Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Dkt. Ntuli Kapologwe anasema mifumo inapounganishwa pamoja na kuweza kuwasiliana inasaidia upatikanaji wa taarifa kwa wakati jambo ambalo linaimarisha utoaji wa taarifa bora na sahihi kwa jamii.

Dkt. Kapologwe anafafanua kuwa katika sekta ya afya kuna mfumo kwa ajili ya takwimu (DHIS2) ambao utawasiliana na Mfumo wa mipango na bajeti (PlanRep) ili kupata viashiria vya utendaji kazi na ufanisi wa sekta ya afya pamoja na mfumo mwingine kwa ajili ya uhasibu na utoaji taarifa kwenye vituo vya kutolea huduma kama zahanati na vituo vya afya (FFARS). Hivyo kwa kuliona hilo Serikali imeamua kuanzisha mfumo wa *Muungano Gateway* ambao utasaidia kuunganisha mifumo yote ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali zitakazotumika katika maamuzi ya vipaumbele katika mipango ya maendeleo .

Anaeleza kuwa muungano wa mifumo yote hiyo na utasaidia upatikanaji wa taarifa moja yenye mnyumbuliko wa taarifa mbalimbali ili kuokoa muda na taarifa ya mfumo mwingine hii inasababisha kupoteza muda, fedha na kazi kuwa ngumu".

Kapologwe anasema mfumo huu utasaidia upatikanaji wa taarifa, takwimu kutoka ngazi zote kuanzia



*Wataalam wa Mfumo wa EPICOR 10.2 kutoka OR-TAMISEMI wakionesha mfumo huo unavyofanya kazi kwa kushirikana mifumo mingine iliyopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Picha: Jacqueline Sombe)*

kuhakikisha upatikanaji wa takwimu ambazo zinajitosheleza. Hili litasaidia watumiaji kutumia mifumo kwa ufanisi na upatikanaji mkubwa wa taarifa sahihi na kuboresha uendeshaji na utoaji huduma bora.

Dkt. Kapologwe anasemaa hii itasaidia kupunguza idadi ya wataalam wa kushughulikia mifumo na kusaidia kupunguza kurudia rudia kazi. "Mfano kuna takwimu ulikuwa unazihitaji kutoka katika mfumo mmoja (DHIS2) kwa kuwa mfumo huo hauongei na mifumo mingine inakubidi kutoa kwanza taarifa hiyo na kuunganisha kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mikoa kwa muda mfupi na haraka pale zinapohitajika kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi tofauti.

Anaendelea kusema mfumo wa *Muungano Gateway* utasaidia utunzaji wa kumbukumbu, kupata taarifa ya mapato, makusanyo pamoja na matumizi yake, taarifa ambazo zinahusiana na idadi ya wagonjwa waliohudumiwa, na upatikanaji wa dawa.

Mfumo pia utasaidia upatikanaji wa taarifa juu ya kiasi gani cha dawa kimepelekwa katika ngazi ya Mkoa au Halmashauri na kiasi gani kimetumika.

***Inaendelea uk. 14***

# Muungano wa Mifumo Suluhu ya Ufanisi katika Vituo vya Kutolea Huduma

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha mifumo inayoisimamia inakuwa na tija na ufanisi kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi. Mabadiliko ya teknolojia katika nchi zilizoendelea na zinazoendela ni suala lisilo epukika na yanaenda



*Erick Kitali, Mkurugenzi wa Idara ya TEHAMA OR TAMISEMI, wakati wa mahojiano Maalum kuhusu Mfumo wa Muungano Gateway Ofisini kwake (Picha: Atley Kuni)*

sambamba na uboreshaji wa mifumo katika sekta ya umma.

Mifumo ambayo imekuwa ikitumika katika Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na vituo vya kutolea huduma imekuwa ikifanya kazi kwa kujitegemea kwa kila mfumo ingawa kiuhalisia mifumo hii inapaswa kufanya kazi kwa kutegemeana.

Mifumo ambayo inategemewa kuunganishwa na kufanya kazi pamoja ni mifumo ya mipango na bajeti (PlanRep), mfumo wa uhasibu na utoaji wa taarifa za fedha katika ngazi ya kituo (Facility Financial Accounting and Reporting System - FFARS), mfumo wa matumizi wa fedha za serikali katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Epicor), pamoja na mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri (LGRCIS).

Ili kuweza kuiwezesha mifumo hii kuwasiliana na kupeana taarifa OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) imefanikiwa kutengeneza programu (software) ijulikanayo kama *Muungano Gateway*.

Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 tayari zimepandishwa kupitia *Muungano Gateway* kwenda EPICOR 10.2, mapato halisi yaliyokusanywa yamekwisha ingizwa kwenye EPICOR na kutoka LGRCIS kupitia *Muungano Gateway*. Mapato na bajeti za jumla ya vituo vya kutolea huduma 24,229 ikiwemo hospitali 85, vituo vya afya 522, zahanati 4796, shule za sekondari 3511 na shule za Msingi 15,315 zimetumwa kwenda FFARS kupitia mfumo huu.

Kaimu, Mkurugenzi Msaidizi, Miundombinu ya TEHAMA OR-TAMISEMI Haji Bamsi, anafafanua kuwa *Muungano Gateway* inauwezo wa kuunganisha mifumo mingi ambayo kwa sasa inatumika hali inayochagiza kuonesha umadhubiti wa mfumo huo na kutoa suluhu ya ucheleweshaji wa taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mfumo mwingine.


> *"Shabaha ni kufikia mifumo ya sekta zote kama vile afya, elimu, kilimo, maji, miundombinu, ambapo itawezesha sasa kuwa na taarifa linganifu kutoka katika kila nyanja mbalimbali," anasema Bamsi.*

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TEHAMA OR- TAMISEMI, Erick Kitali, anaeleza kuwa jukumu kubwa la Wizara nikuhakikisha *Muungano Gateway* inafanikiwa na kuwa na takwimu sahihi ambazo zitatoa taarifa zitakazowezesha kufanya maamuzi sahihi sambamba na kushirikiana na idara na sekta zingine

"Kwa kushirikiana na wadau kama Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), OR-TAMISEMI, tunataka *Muungano Gateway* ifike mahali tunakuwa na Dashibodi moja ambayo itaunganishwa katika mfumo huu na

**Inaendelea uk. 9**

# Muungano wa Mifumo Suluhu ya Ufanisi




*Mchoro unaoonyesha jinsi Muungano Gateway inavyounganisha mifumo iliyopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa*

*(Mchoro: Maktaba)*

***Inatoka uk. 8***

baada ya hapo takwimu zitakazokuwa zinapatikana katika kila ngazi ziwe zinatumika katika shughuli za kila siku hususani katika utoaji wa maamuzi" anaongeza Kitali.

Kitali anafafanua kuwa OR-TAMISEMI inafika hadi kwenye ngazi zote za msingi na kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta kama Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais Utumishi kuhakikisha hata mifumo iliyopo sehemu zingine inafungamanishwa na *Muungano Gateway.*

"*Muungano Gateway,* itazuia makosa ya kujirudiarudia au kutoa taarifa tofauti-tofauti hivyo tunachotaka kufanya nikuunganisha hata mifumo mingine ya wizara na idara nyingine za serikali kwa lengo la kumhudumia Mtanzania" anaeleza Kitali.

Mkurugenzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka PS3 anaeleza kuwa mfumo unazingatia si utaoaji wa taarifa tu bali taarifa zinaziokidhi mahitaji.

Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kushirikiana na mradi wa PS3, kwakutumia wataalam wa ndani wamefanikiwa kukamilisha mfumo wa *Muungano Gateway* utakaounganisha mifumo mingine yote ya hapo awali na kurahisiha utendaji wa kazi sambamba na kutoa taarifa sahihi na kwa wakati na kuboresha huduma.

> *"Dhumuni kuu ni kusaidia watumiaji katika ngazi tofauti kufanya kazi kwa mifumo mizuri na kuwa na urahisi wa kupata taarifa zenye viwango zitakazopelekea kuwa na ufanisi, usimamizi uli-oboreshwa and utoaji huduma" anasema Wengaa*

***Atley Kuni, TAMISEMI na Jacqueline Sombe, PS3***

# *Muungano Gateway* Msingi wa Taratibu na Kanuni za Mifumo

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), kwa kushirikiana Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma PS3 imeendelea na jitihada za kuhakikisha kunakuwa na mifumo imara na madhubuti kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali.

Afisa Msimamizi wa Fedha Ummy Wayayu, kutoka OR-TAMISEMI, anasema utaratibu wa kupanga lazima uanzie ngazi ya msingi kwa jamii kuchambua na kuamua vipaumbele vyao kama sheria inavyotaka baada ya Halmashauri kupokea ukomo wa bajeti (Ceiling), ambayo hutumika kama muongozo wakati wa upangaji wa mipango na bajeti.

Wayayu anaendelea kusema kuwa katika bajeti ya mwaka 2018/19, uhalisia wakuhusisha ngazi ya msingi umejidhihirisha kwa kufuata hatua za uandaaji wa bajeti kuanzia ngazi ya Halmashauri na hatimaye Mkoani kabla ya kuwasilishwa Wizarani kwa uchambuzi zaidi kwa njia ya kieletroniki *"Centralized and Web-based System"*.

Anaendelea kusema mara baada ya kuwasilisha bajeti husika, huingizwa kwenye mfumo wa Matumizi wa Halmashauri (Epicor) kwa ajili ya utekelezaji kwa kipindi husika. Fedha zote kwaajili ya matumizi zipo katika akaunti za pamoja zilizopo Benki Kuu, ambapo kwa kutumia mfumo wa (Treasury Single Account) kila Halmashauri inatumia kadiri ya fedha iliyonazo na haiwezi kutumia fedha za halmashauri nyingine,

Wayayu anafafanua kwamba *Muungano Gateway* itafanya mifumo iwasiliane na kubadilishana taarifa, siku zote taratibu za kifedha zipo pale pale lakini kwa suala la ukuaji wa teknolojia kuwasiliana kwa mifumo ni maendeleo ambayo hata kwetu wahasibu tumerahisishiwa sana hasa suala la uaandaaji wa taarifa.

Anasema kuwa, kutokana na changamoto zilizoanishwa, *Muungano Gateway* imeundwa kuunganisha mifumo ili kutatua changamoto ya mifumo kushindwa kupeana taarifa.

"Nawasisitiza Maafisa Mipango na Waweka Hazina kuhakikisha wanatumia fedha kulingana na kifungu kilichopangwa kwa kuhakikisha wanapoanza kufanya matumizi kuwe na ulingano ili kuepusha mfumo kukataa. Maafisa wanaohusika na mipango pamoja na watumiaji wengine wote wa mifumo katika Halmashauri wanatakiwa wafuate taratibu hizo. Kumekuwa na malalamiko kadhaa mfano bajeti inaainisha matumizi fulani lakini maafisa wanaelekeza kwenye matumizi tofauti. Hii mfumo utakataa, hivyo ieleweke katika hali ya sasa teknolojia haidanganyi, tumia kama ulivyopanga," anasisitiza Wayayu.

Vitus Kakoko, Mhasibu Idara ya TEHAMA, OR-TAMISEMI anaongeza kuwa, mifumo kabla ya kuunganishwa na *Muungano Gateway*, ilifanya kazi kila mmoja kivyake na hata wakati wa uandaaji wa taarifa kila taarifa iliandaliwa kivyake, jambo ambalo lilitumia muda mwingi katika kukusanya na kuunganisha taarifa.

"*Muungano Gateway*, imeunganisha mifumo muhimu ambayo taarifa zake zinategemeana, hivyo sasa itakuwa rahisi sana kuweza kupata taarifa hizo sababu mifumo hii inavyoongea imewezesha taarifa nyingine kupelekwa moja kwa moja kwa kila mara zinapoingizwa na mfumo mwingine," anasema Kakoko.

Naye Peter Ngallya Afisa kutoka Idara ya TEHAMA OR- TAMISEMI, akifafanua juu ya utaratibu unaofuatwa katika Mfumo wa FFARS, ipo moduli inayofahamika kama Mipango na Bajeti (Planning and Budgeting) ambayo hutumika katika suala zima la kupanga mipango na bajeti ya vituo vya kutolea huduma kwa kusimamiwa na wataalam wa Halmashauri.

***Inaendelea uk. 15***



***Ummy Wayayu, Afisa Msimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Mamlaka za Serikali za Mitaa sehemu ya usimamizi wa fedha, akitoa majibu mbele ya Mwandishi kuhusu kanuni zinazoongoza wakati wa kuandaa bajeti lakini pia wakati wakufanya matumizi. (Picha : Atley Kuni)***

# Matumizi ya Mifumo Yaokoa Zaidi ya Milioni 15 Kongwa

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Mkoani Dodoma imefanikiwa kupunguza gharama za matumizi kutoka kati ya shilingi milioni 24 na 30 hadi kufikia milioni 5 ikiwa ni gharama za matumizi ambazo zimekuwa zikitumika wakati wa zoezi zima la uandaaji wa bajeti za mwaka wa fedha za Halmashauri kabla ya kuanza kutumia mifumo iliyoboreshwa.

Gharama hizo zilijumuisha usafiri (mafuta na service za magari) posho za



*Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Agnes Bitina Kabuje akiingiza vocha za malipo katika mfumo wa EPICOR 10.2 (Picha : Jacqueline Sombe)*

watumishi, kununua makaratasi, pamoja na vifaa vingine ambavyo vinatumika katika zoezi la uandaaji taarifa na uwasilishaji wa bajeti kwenda Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI).

Akieleza mafanikio hayo Mhasibu wa Matumizi wa Halmashauri ya Kongwa Fabian Mayingu anasema "matokea hayo ni kutokana na uboreshwaji wa mifumo katika ngazi ya Halmashauri na vituo vya kutolea huduma ambapo mifumo kama PlanRep, Epicor, FFARS na LGRCIS imeboreshwa kwa kuiwezesha kuongea na kupeana taarifa kwa njia ya kielektoniki hivyo kuiwezesha serikali kuokoa gharama kubwa za matumizi zilikuwepo awali kabla ya mifumo."

"Badala ya kuzunguka na makaratasi kwenye korido za halmashauri, kila Mkuu wa Idara sasa anaweza kutuma moja kwa moja mpango wake wa bajeti kwa Afisa Mipango ambapo naye hutuma moja kwa moja OR-TAMISEMI, baada ya mchakatako wa bajeti kupitishwa na serikali, TAMISEMI huurudisha mpango kwetu kupitia mfumo wa Epicor kwaajili ya kufanya matumizi hapa halmashauri na kwa vituo vya kutolea huduma wao hupata mpango kupitia FFARS, hilo limefanyika hapa Kongwa" Alisema Mayingu.

Mayingu anaendelea kusema kuwa watumishi wakiendelea kuitumia mifumo na kuizoea gharama za matumizi katika uandaaji wa bajeti utapungua zaidi na hivyo Serikali kupunguza gharama za uandaaji wa bajeti katika ngazi ya Halmashauri.

Kwa upande wake Mtakwimu (Afisa Mipango) Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Frank Uhwello, anaeleza kuwa kumekuwa na faida kubwa kwa upande wa Idara yao inayosimamia mipango na bajeti tangu mifumo ilipoanza kufanya kazi katika Halmashauri ambapo imeweza kuongea na kupeana taarifa hususani wakati wa maandalizi hadi uwasilishwaji wa bajeti.

"Badala ya kufanya kazi mara mbili ya kutuma taarifa kutoka PlapRep kwenda Epicor, ilibidi OR-TAMISEMI kuhamisha taarifa kwenda kwenye 'microsoft excel' kuipanga katika vyanzo vya kila fedha, kulingana na mahitaji ya mfumo na baada ya hapo ndio kuihamisha kwa kutumia njia ya vitabu 'manually' kwenda Epicor, lakini kwa sasa inaenda taarifa zinakuja moja kwa moja kupitia mfumo wa Epicor" anaongeza Uhwello.

Kuhusu PlanRep kuwasiliana na FFARS hapo awali bajeti zote katika ngazi za vituo vya kutolea huduma ilikuwa inafanyika Halmashauri na kupangwa na kutekelezwa na Halmashauri wakati bajeti ni jambo la kushirikiana na kila muhusika kushiriki, kuyatolea maoni au kueleza vipaumbele.

Mwanzo hilo lilikuwa linafanyika kwa kufanya makadirio tu, lakini kwa sasa wanashirikishwa katika mipango yote na wana uwezo wa kuona kupitia FFARS moja kwa moja.

***Inaendelea uk. 15***

# Mifumo Thabiti Mhimili wa Huduma Bora kwa Wananchi

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi za umma kwa lengo la kutoa huduma bora kwa haraka, kwa gharama nafuu na zinazopatikana wakati wote, ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji.

Uwezo wa mifumo kupeana taarifa ndio msingi wa kuelewa mabadiliko katika kuelekea kuwa na Serikali Mtandao iliyo thabiti. Kuna mifumo mingi mizuri ndani ya serikali ambayo ina manufaa lakini ni michache sana kati yao ambayo ina uwezo wa kuwasiliana na kupeana taarifa au imekosa jukwaa la pamoja ambalo mifumo ina uwezo wa kutuma na kupokea taarifa ambazo wananchi wanashirikishwa.



*Wauguzi katika moja ya hospitali nchini wakitoa huduma kwa wananchi kwa kutumia mfumo wa kieletroniki wa GoTHOMIS (Picha: Maktaba)*

Mkurungenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Erick Kitali anaeleza ni kwa jinsi gani mifumo inapowasiliana na kupeana taarifa inafanikisha mpango wa Serikali Mtandao unaolenga wananchi.

“Katika kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia TEHAMA tumepanga kufanikisha uwajibikaji, uwazi, kuzingatia utawala wa sheria na usawa kwa kuwa mifumo inapowasiliana na kupeana taarifa inasaidia wananchi kufahamu mambo mbalimbali yanayoendelea katika maeneo yao,” anasema Kitali

Kitali anaongeza kuwa mwanachi wa kawaidia anataka kujua nini kimepangwa, bajeti zikoje, matumizi yamefanyikaje, kwa hiyo kama mwanachi na wadau wengine wanafuatilia kujua na kufahamu kinachoendelea, wataweza kupata taarifa hizo kupitia dashibodi iliyopo katika *Muungano Gateway* inayomwezesha kupata taarifa zinazohitajika kwa wakati na uwazi.

“Muungano wa mifumo utasaidia kuchochea utoaji wa huduma kwa wananchi kwa mfano mwanachi anataka kujua huduma gani inatolewa na taasisi gani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwani *Muungano Gateway* inaunganisha mifumo mbalimbali kama ilivyo www.tanzania.go.tz ambapo mwananchi anaweza kupata taarifa na kuuliza maswali ya huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali za Serikali.

Akiongelea kuhusu mipango ya baadae juu ya namna gani muungano wa mifumo inachochea Serikali mtandao kwa kuwezesha wananchi kupata taarifa muhimu kutoka taasisi mbalimbali za serikali kama vile NIDA na TRA, Kitali anasema muungano wa mifumo itasaidia kupata taarifa mbalimbali kwa wakati, na kuokoa muda hivyo itasaidia kukuza uchumi wa nchi kwa kuwa kazi ambazo zilikuwa zinafanywa kwa siku nyingi kukamilika kwa muda mfupi na kusababisha baadhi ya shughuli zingine za kukuza pato la nchi kufanyika

Anasema serikali pia imeweka mkazo katika serikali mtandao kwani inatumika kama chombo au chanzo cha kuwaleta wananchi karibu na serikali yao, kushiriki katika mipango na bajeti za maeneo yao, kufahamu matumizi yanayofanyika na kufuatilia ripoti zinatolewa.

Kitali anasema lengo la serikali mtandao ni kutoa huduma kwa wananchi ambayo itafanikisha kuwepo kwa jukwaa la ushirikishwaji wa taarifa na hivyo kuepuka vitendo vya rushwa pamoja na urasimu ambao mara kwa mara umekuwa ukionekana hapo zamani wakati mfumo haukuwepo.

Hata hivyo anaeleza kuwa mkakati mwingine wa OR-TAMISEMI ni kuboresha mifumo inayozingatia utawala bora na inayotambulika kimataifa ambayo hutegemeana kwa njia ya kielektroniki ikienda sambamba na ulimwengu wa Kiteknolojia.

Anaeleza kuwa kuimarisha serikali mtandao kupitia *Muungano Gateway* pia kutachangia kukuza na kuitangaza vyema taaluma ya TEHAMA ambayo ulimwenguni kwa sasa inashika kasi kutokana na uwezo wa kurahishisha mambo mengi katika jamii kama kupunguza gharama za uendeshaji ambayo kwayo itaongeza uwezo wa serikali kutoa huduma bora kwa manufaa kwa wananchi.

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

# Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji Warahisishiwa Upatikanaji Taarifa

Uunganishwaji wa mfumo ulioimarika hauna budi kutoa taarifa zilizoboreshwa ambazo zina manufaa kwa taasisi husika, wananchi wanaotembelea kwenye taasisi kupata taarifa na wananchi wanaohudumiwa kupitia tovuti za wizara, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Moja ya jitahada za kuboresha utoaji wa taarifa zilizo sahihi na kwa wakati Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikao, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu NBS, UNICEF na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kwa pamoja wamefanikiwa kukusanya mahitaji ya wadau na viashiria kutoka katika wizara za kisekta (mwezi februari 2018) na kufuatiwa na usanifu wa Mfumo jumuishi wa kieletroniki wa ufuatiliaji na tathmini (Intergated Monitoring and Evaluation-iMES) mwezi Aprili 2018.

iMES (Intergrated Monitoring and Evaluation) ni miongoni mwa mfumo unaounganishwa na mifumo mingine iliyopo kupitia Muungano Gateway.

Mfumo jumuishi wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini (iMES) ni mfumo utakaounganishwa na mifumo mingine ya kisekta ili kuchukua taarifa ambazo tayari zimeshakusanywa na mifumo hiyo, pia itakuwa na uwazi wa kukusanya taarifa nyingine ambazo hazikusanywi na mifumo yeyote. iMES inaunganisha taarifa kutoka kwenye mifumo mbalimbali iliyoko kwenye Muungano Gateway na wizara za kisekta ambazo zitakuwa ni taarifa sahihi.

Mifumo hiyo inaboreshwa na kuwa ya kielektroniki na kuwa *web-based*. Kunapokuwa na jukwaa moja la mifumo na mawasiliano ya mifumo yaani (*systems interoperability*) kwa wakati mmoja inarahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati hivyo kuepusha mkanganyiko wa taarifa.

Akihojiwa kuhusu Mfumo wa IMES Mtakwimu kutoka OR-TAMISEMI, Elgiva Florence anasema kuwa mfumo huo una lengo la kufuatilia programu, kazi zinazofanywa na Wizara yaani OR-TAMISEMI na Wizara za Kisekta na ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali ili kuweza kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza mfano katika ujenzi unaoendelea wa vito vya afya na madarasa.

"Matarajio ya mfumo huo ni kurahisisha upatikanaji wa taarifa zili zo sahihi na kwa wakati kutoka kwenye chanzo kinachoaminika. Kulikuwa na mfumo wa Local Government Monitoring Database (LGMD) mfumo huu ulikuwa hauingiliani na mfumo mwingine ulikuwa unakusanya taarifa kutoka kwenye Halmashauri na kutumia makaratasi kwa ajili ya kukusanya taarifa jambo ambalo haikuwa rahisi kupata taarifa kwa wakati mmoja hivyo kila sekta ilikuwa inatoa taarifa kila mmoja kivyake na ilikuwa ngumu kuandaa taarifa tofauti kwa wakati mmoja," anasema Elgiva

Anafafanua kuwa mfumo huo utaleta ufanisi na kuongeza upatikanaji wa taarifa, uwazi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuwa watu wataweza kupata taarifa kwa urahisi na kwa muda wote anaohitaji

zoezi la ufuatiliaji na tathmini kulingana na mahitaji ya wadau ikiwepo OR-TAMISEMI Wizara za Kisekta, Sekretaieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wananchi.

***Inaendelea uk. 16***



***Watakwimu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mathias Coster na Elgiva Florence wakieleze jinsi Muungano Gateway itakavyosaidia mifumo kuboresha utoaji wake wa taarifa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Picha: Jacqueline Sombe)***

# *Muungano Gateway:* Chanzo cha Maamuzi ya Kiutendaji Serikalini

***Inatoka uk. 7***

Vilevile itasaidia watumishi wa ngazi za msingi wanapopanga bajeti mipango yao iwe rahisi kuweza kufanyia maamuzi ya kiutendaji katika kuchanganua mahitaji na kutoa vipaumbele.

Anasema itasaidia kujua idadi ya watumishi waliopo nchini nmgawanyo wake kwa kada na kwa maeneo ya mjini na vijijini. Mfumo pia utawezesha kujua ni idadi gani ya watumishi wanaohitajika na maeneo wanayohitajika, hitaji la watumishi, mapungufu yaliyopo pia katika suala zima la kuajiri. "Wenzetu walioko katika Halmashauri na ngazi ya Mikoa wapokee mifumo na kuwa tayari kutekeleza kwa kuwa wao ndio watendaji wakuu, OR– TAMISEMI wanaratibu hivyo wanajukumu kubwa la kuhakikisha mifumo inatekelezwa na kufanikiwa kwa kiwango kinachotakiwa," anaeleza Dkt. Kapologwe

Anaendelea kusema kuwa *Muungano Gateway* utasaidia kuwepo kwa uhalisia wa bajeti, utachangia kutokuwepo kwa upotevu wa taarifa kama ilivyokuwa awali na kuhakikisha kwamba mipango na bajaeti kuanzia ngazi ya zahanati mpaka Wizara zinapangwa kulingana na uhitaji wa maeneo husika.

Anafafanua kuwa hii itasaidia kuwepo kwa usahihi wa taarifa tofauti na awali ambapo kupata taarifa moja ilikuwa ni shida mfano kupata taarifa ya mapato ili iweze kutumika katika mfumo wa matumizi ilikuwa lazima ifanywe kwa njia ndefu kupitia vitabu. Ililazimu kutengeneza faili pembeni na kuliingiza tena kwenye matumizi ambapo hili lilikuwa linapelekea kutokuwa na taarifa sahihi za mapato na matumizi hivyo kwa kutumia *Muungano Gateway* mifumo hiyo itawasiliana hivyo taarifa itakuwa na uhalisia.

Hata hivyo Afisa TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, Haji Idd analeza kuwa zipo faida nyingi kwa kuwepo na njia moja inayowezesha mifumo kuwasiliana hasa katika kuhakikisha huduma zinaboreshwa katika jamii. Mojawapo ni taarifa ya fedha, mipango, mkusanyo na matumizi zitaboreka tofauti na awali ambapo ilikuwa ikipatikana katika mifumo tofauti lakini kwa kutumia Muungano Gateway taarifa hizo zinaweza kuunganishwa na kuweza kupatikana ili kurahisisha kazi wakati wa kufanya maauzi yanayochangiwa na kuwepo kwa taarifa hizo.

Idd anaendelea kufafanua kuwa itarahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za fedha katika ngazi mbalimbali za maamuzi kuanzia kwenye mikoa, halmashauri na wizara ili kuweza kufuatilia namna halmashauri zinavyoweza kukusanya na kutumia fedha na kuangalia jinsi vipaumbele vinavyoweza kufanyiwa kazi.

Anamaliza kwa kusema kuwa *Muungano Gateway* kwa upande wa watumiaji hasa watumishi inaongeza ufanisi wa kufanya kazi hivyo muda mwingi waliokuwa wakitumia kutengeneza bajeti, kuhamisha, kukaa muda mrefu unaweza kutumia kufanya kazi nyingine.




***Wataalam wa TEHAMA, Anatory Antidius na Vitus Kakoko wa OR-TAMISEMI, wakiwa wanapitia makusanyo yaliyopitia katika mfumo wa LGRCIS tayari kwenda Epicor kupitia 'Muungano Gateway' kwa ajili ya kuanza kutumika. (Picha: Atley Kuni)***

***Angela Msimbira,***
***TAMISEMI***

# *Muungano Gateway* msingi wa taratibu na kanuni za mifumo

***Inatoka uk. 10***

"Kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 wataalam katika ngazi ya kituo wamefanya bajeti zao kupitia mfumo wa mipango na bajeti (PlanRep) na baada ya kukamilisha kazi hiyo, mipango na bajeti zao zimeingizwa kwenye mfumo wa FFARS kupitia *Muungano Gateway* tofauti na zamani ambapo walifanya mipango na bajeti zao kwenye mfumo wa FFARS pekee hivyo uwepo wa *Muungano Gateway* imewezesha mifumo kubadilishana taarifa," anaeleza Ngallya.

Ngallya pia anasema kupitia Muungano Gateway, PlanRep huweza kulisha taarifa mifumo mingine kama Epicor ambayo hufanya matumizi ngazi ya Halmashauri, FFARS matumizi ngazi ya kituo na mfumo wa makusanyo ya ndani (Local Government Revenue Collections Information System - LGRCIS) ngazi ya Halmashauri aidha mfumo wa Muungano *GateWay* una uwezo kuunganisha mifumo zaidi kutoka Wizara nyingine za kisekta.

Aidha ili mfumo wa *Muungano Gateway* na mifumo mingine yote ifanikiwe kutoa huduma bora kwa wakati, OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na PS3 wameweka dawati maalumu la kuwezesha huduma za kiufundi kuanzia ngazi ya Wizara, Mkoa na Halmashauri ambalo linapatikana ndani ya mtandao wa OR-TAMISEMI kupitia http://helpdesk

Ngallya pia anasema kupitia Muungano Gateway, PlanRep huweza kulisha taarifa mifumo mingine kama Epicor ambayo hufanya matumizi ngazi ya Halmashauri, FFARS matumizi ngazi ya kituo na mfumo wa makusanyo ya ndani (Local Government Revenue Collections Information System LGRCIS) ngazi ya Halmashauri aidha mfumo wa Muungano Gate Way unauwezo kuunganisha mifumo zaidi kutoka Wizara zingine za kisekta.

Aidha ili mafanikio ya mfumo wa Muungano Gateway uweze kufanikiwa, OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na PS3 wameweka dawati maalumu lakuwezesha huduma za kiufundi kuanzia ngazi ya Wizara, Mkoa na Halmashauri.

***Atley Kuni, TAMISEMI***

## Matumizi ya mifumo yaokoa zaidi ya milioni 15 Kongwa

***Inatoka uk. 11***

"Mifumo hiyo imeweza kuokoa muda wa kufanya kazi, ambapo kama imepangwa kufanyika ndani ya siku nne, itamalizika kwa siku nne wakati awali kazi kama ilipangwa siku nne haikuwa rahisi kuimaliza ndani ya siku nne kutokana na changamoto ambazo zilikuwa nje ya uwezo wetu," anaeleza Uhwello.

Uhwello anamaliza kwa kusema kuwa usalama wa taarifa na usawa umeongezeka sana kupitia mifumo kuunganishwa na kuwasiliana. Kwa jinsi mifumo ilivyokuwa inafanya kazi zamani ilikuwa inapofika mwisho wa kufanya bajeti bado kulionekana kuwa kuna makosa katika taarifa, zilikuwa zinarudishwa na mchakato kutumia muda tena kurekebisha mipango na bajeti iliyoingizwa, tofauti na sasa ambapo kuna usimamizi thabiti kwenye mfumo ambapo marekebisho yanafanyika kwa haraka.

OR- TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 wanafanya juhudi ya kuhakikisha mifumo inawasiliana na kupeana taarifa kupitia *Muungano Gateway* ambapo inaiwezesha serikali kupunguza gharama kubwa za matumizi na kwa hilo fedha zinaweza kuelekezwa katika mipango mingine ya maendeleo ya wananchi.

***Jacqueline Sombe, PS3***

# Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji warahisishiwa upatikanaji taarifa

***Inatoka uk. 13***

"Mfumo utasaidia wakati wa taarifa ya elimu au afya kutakuwa na Dashibodi ambayo itamuonesha moja kwa moja takwimu anazozihitaji na itapunguza gharama ya upatikanaji wa taarifa. Mfumo huu pia utapunguza gharama (muda wa fedha) safari za kutafuta taarifa hizo katika sekta husika na urasimu wa upatikanaji wa taarifa.

Mfumo utakuwa na ripoti mbalimbali zenye taarifa za kitakwimu ambazo zinaonesha wasifu wa kijamii na kiuchumi (Social Economic Profile) zilizopo katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri, taarifa zinapatikana katika Dashbodi ambayo kila mmoja ataweza kuzipata moja kwa moja.

Eligiva anasema mfumo utaweka uwazi wa matumizi ya Fedha na kutoa repoti ya "*Public Financial Management (PFM)*" na kuweza kupata ripoti mbalimbali za Wizara za kisekta mfano elimu, afya na *"Perfomance M&E Report"* kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini kupitia mahusiano yaliyopo katika viashiria mbalimbali ambapo wahusika watakuwa wanapata taarifa mbalimbali za kitakwimu

Anaendelea kusema kuwa mfumo huu utahusisha viashiria vingi na vitakuwa vimesheheni taarifa mbalimbali ambazo mtu yeyote anaweza kupata taarifa kwa uwazi pia itarahisisha kufanya mahusiano katika viashiria mbalimbali kwa kuangalia jinsi vinavyouhusina katika kila mmoja. Mfumo utamsaidia mdau yeyote ambaye anahitaji kufanya utafiti katika eneo fulani mfano magonjwa ataweza kupata taarifa zitakazo muwezesha kufanya maamuzi kwakuwa mfumo utamuonesha maeneo ya kimkakati kwaajili ya tafiti hiyo.

Aidha mfumo utafanya kazi kwa kuzingatia sera ambazo zitasaidia kutoa huduma sahihi na huduma bora kwa wananchi.

***Angela Msimbira, TAMISEMI***

# Uwiano Sahihi wa Taarifa za Fedha katika Halmashauri Waimarishwa

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), kwa mara ya kwanza imeamua kurahisisha shughuli za kiserikali zilizokuwa zikifanywa kwa njia ya mifumo ya zamani (manual) ya kutuma na kupokea taarifa za mapato na bajeti za Halmashauri, na kuwa kwa njia ya kielektoniki kupitia *Muungano Gateway*.

> *Muungano Gateway* ni mfumo wa Serikali unaowezesha mifumo mingine kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Kwa kutumia wataalam wa ndani ya nchi, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3), iliamua kutengeneza mfumo wa *Muungano Gateway*, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kurahisisha mawasiliano baina ya mifumo ya ndani ya OR-TAMISEMI, wizara za kisekta na wadau wanaohitaji taarifa.

Afisa wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka OR-TAMISEMI, James Mtatifikolo, anaeleza kwamba *Muungano Gateway* ina lengo la kuwezesha mifumo yote kuwasiliana ili kuweza kupata taarifa mbalimbali zinazofanyika katika wizara, wizara za kisekta, wadau, Halmashauri na Mikoa.

Anasema kwamba hadi sasa mifumo iliyounganishwa katika *Muungano Gateway* ni mfumo wa mipango na bajeti (PlanRep), ambao unasaidia mipango na bajeti za vituo vya kutolea huduma kwa wananchi kuonekana hivyo unachochea kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa wananchi wa Tanzania.

Mfumo mwingine ambao umeunganishwa ni wa uhasibu na utoaji wa taarifa za fedha katika ngazi ya kituo (FFARS). Kupitia mfumo huu vituo vyote vya kutolea huduma hukukusanya na kuhifadhi taarifa za mapato na matumizi zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya vituo hivyo, ili wananchi waweze kunufaika na raslimali fedha kwa kupatiwa huduma bora.

Mtatifikolo anaongeza, mfumo mwingine ni wa matumizi wa fedha za Serikali katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Epicor), huu ni mfumo wa usimamizi wa fedha za umma katika toleo la 10.2 (Epicor 10.2), mifumo yote ya msingi ya usimamizi wa fedha katika sekta za umma kwa sasa itaweza kuwasiliana na kupeana taarifa.

***Inaendelea uk. 17***

# Uwiano Sahihi wa Taarifa za Fedha Waimarishwa




*James Mtatifikolo Afisa TEHAMA, akifanya mawasilisho ya mfumo wa PlanRep ambao kwa sasa utaweza kufanya kazi na mifumo mingine kupitia Muungano Gateway (**Picha: Atley Kuni**)*

***Inatoka uk. 16***

Hapo awali, uongozi na maafisa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa walilazimika kupitia mipango na bajeti katika mfumo mmoja, mapato katika mfumo mwingine na matumizi kwenye mfumo mwingine, hivyo kuleta ugumu katika kudhihirisha uwajibikaji, ufanisi na thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za Serikali.

Anasisitiza mipango na bajeti ikifanyika kwa njia ya mifumo, suala ubadilishanaji wa taarifa kwa mifumo iliyopo ndani ya OR-TAMISEMI na serikali kwa ujumla nalo lazima lifanyike kieletroniki kwa kuwa ni rahisi na linaokoa muda na rasimali ambazo zitaelekezwa kwenye shughuli zingine za maendeleo lakini pia upatikanaji wa taarifa utakuwa rahisi, sahihi na kwa wakati kama *Muungano Gateway* ilivyotumika ipasavyo katika mapato, mipango na bajeti ya mwaka huu.e

"Pamoja na mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri (LGRCIS), ambao ni muhimu sana katika Halmashauri nchini. Mfumo huu wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato umewezesha mapato ya ndani kuongezeka kwasababu umezuia upotevu wa fedha ambao ulikuwa unatokea hapo awali wakati wa kutumia vitabu katika kumbukumbu za fedha. Mfumo huu ni madhubuti na unasaidia kukuza pato katika Halmashauri na kuweza kujitegemea na pia kuzalisha pato la taifa kwa ujumla," anaeleza Mtatifikolo.

Anaeleza kuwa, mifumo hii ni msingi katika mapato na matumizi ya Halmashauri kuanzia ngazi za chini za msingi yaani vituo vya kutolea huduma. Mifumo imeweza kuhuishwa ili iweze kuzungumza kwa pamoja kwakuwa taarifa zake zinategemeana na hivyo ili kusaidia kurahisisha utendaji kazi wake, TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 imeleta *Muungano Gateway* kama njia ya kurahisisha mifumo hii kuweza kutuma taarifa zinazotegemeana na kwa haraka zaidi.

Mtatifikolo anaeleza kuwa, uimara wa makusanyo, mipango, bajeti na matumizi, inatokana na kuwa na mifumo thabiti ambayo ni mfumo wa mipango na bajeti (PlanRep), mfumo wa uhasibu na utoaji wa taarifa za fedha katika ngazi ya kituo (FFARS), mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri (LGRCIS ) na mfumo wa matumizi ya fedha za Serikali katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Epicor) ili kujua mapato yaliyokusanywa, kupangwa na zilivyotumika, ambapo huwasiliana moja kwa moja kupitia *Muungano gateway.*

Mtatifikolo anasema mfumo wa *Muungano Gateway* umesanifiwa na wataalam wa ndani ya Serikali na hususani watumishi walio chini ya OR-TAMISEMI na wadau wa maendeleo PS3 jambo ambalo litakuwa rahisi kuhudumia mfumo hata baada ya mradi kumaliza muda wake.

***Atley Kuni, TAMISEMI***